CHUKA UNIVERSITY
Knowledge is Wealth / Akili ni Mali *(Sapientia divitia est)*
020 200 8549
library@chuka.ac.ke
www.chuka.ac.ke
P.O Box 109 - 60400, Chuka
www.chuka.ac.ke | chuka university official | ChukaUniversityOfficialPage | chuka_uni
OUR CORE VALUES: Freedom of Expression | Integrity | Sustainability | Teamwork | Excellence and Professionalism | Confidentiality
library@chuka.ac.ke; www.chuka.ac.ke

# CONTRIBUTION OF THE NEW CONSTITUTION IN PROMOTING KISWAHILI USE IN MASS MEDIA

***Mugambi, A.***
*Department of Arts and Humanities, Chuka University, P. O. Box 109, Chuka*
*Email: mugambi2050@gmail.com, Tel. 0721342296*

Citation:
***Mugambi, A. (2015)*** Contribution of the New Constitution in Promoting Kiswahili Use in Mass Media. In: Isutsa, D.K. and Githae, E.W. *Proceedings of the First International Research Conference held from 29th to 31st October, 2014 in Chuka University, Chuka, Kenya.180-187pp.*

## ABSTRACT
Media plays a major role in the society; it is the medium of providing information, it creates social integration, and promotes shared values, knowledge and entertainment. Proper use of standard language is essential to achieve these objectives. Media industry in Kenya has grown exponentially from the early 1990s. This growth has been characterized by the deployment of the latest technological innovations, increased number of frequency modulated radios and professional media practitioners. Many of the media houses in Kenya today are using different styles and methods to attract and keep listeners for their own economic survival. This paper investigates the effects of new constitution on the language used in the mass media. It highlights the gains that have been made specifically in promoting Kiswahili language as a national and official language as well as the challenges.

## IKISIRI
Vyombo vya habari vinatekeleza majukumu mengi katika jamii. Hata hivyo jukumu la kimsingi ni kupasha habari kwa hadhira pana inayosikiliza. Kufanikisha jukumu hili kwa umma ni muhimu kuzingatia lugha sanifu na sahihi (Walibora, 2001). Sababu ya kutumia lugha sanifu ni kufanikisha upashaji wa habari kwa watu wote. Kutokana na hali hiyo vyombo vya habari vina jukumu la kimsingi la kutumia lugha sanifu katika utoaji wake wa habari. Aidha, kutokana na upana wake wa hadhira, vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja (Mohochi, 2006). Wataalamu wengi wa lugha vilevile wanaviamini kuwa kama nyenzo ya kukuza lugha (Chimerah, 2000; Mulokozi, 2003).

Siku za hivi karibuni kumekuwa na vyombo vingi vya habari. Hali hii imechangiwa na kasi na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Teknolojia hii imepunguza umbali kupitia mawasiliano na kuunganisha ulimwengu mzima kiasi kwamba dunia sasa imekuwa kama kijiji kidogo. Karne ya 21 imekuwa ni karne inayotambulikana zaidi kupitia matumizi mapana ya teknolojia ya mawasiliano. Nchini Kenya, uzinduzi wa katiba mpya katika mwaka wa 2010 ulifungua ukurasa mpya na kusababisha msisimko mkubwa miongoni mwa wataalamu wa lugha na wakereketwa wengine. Sababu ni kwamba katiba hii ilitoa uhuru mwingi wa upataji wa habari pamoja na mawasiliano na kuondoa vikwazo vilivyokuwepo hapo awali. Aidha lugha ya Kiswahili ilipewa majukumu mawili kama lugha rasmi kwa mara ya kwanza nchini pamoja na kuendelea kuwa lugha ya taifa. Masuala haya ndiyo yalichochea utafiti huu ili kuchunguza iwapo athari za katiba mpya katika lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari ni hasi au chanya hasa katika upande wa matumizi ya lugha sanifu.

Makala hii ililenga kuchunguza athari ya katiba mpya kwa lugha ya Kiswahili na jinsi Kiswahili kinavyotumika katika vyombo vya habari. Hoja muhimu iliyoendelezwa hapa ni kuwa katiba mpya imechangia kukuza na kupanua lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari. Kwa upande wa pili, hali hii imeleta changamoto kwa kuathiri mbeko za uzingatifu wa Kiswahili sanifu huku vyombo vya habari viking’ang’ania kutumia uhuru wa kikatiba uliotolewa na katiba mpya na kuvunja sheria za lugha sanifu. Katika kufanya hivi vyombo vya habari vimeibua mitindo mingi

ya matumizi ya lugha isiyo sahihi na kuwaudhi wapenzi wanaosikiliza Kiswahili huku ikiwapotosha wengine. Nadharia ya uchanganuzi makosa kwa mujibu wa Corder (1967) iliongoza utafiti wa makala hii. Mbinu za utafiti zilizotumika ni jedwali la tathmini pamoja na hojaji kwa wana habari. Mtafiti alisikiliza taarifa za habari kutoka idhaa za redio za *Citizen* na *Idhaa ya Taifa* (KBC) mtawalia kwa muda wa miezi mitatu. Baadaye alirekodi makosa yaliyopatikana pale na kuyachanganua. Ilibainika kwamba idhaa za utangazaji zilikuwa na makosa mengi ya kisarufi kama vile uchanganyaji ndimi, ukosefu wa upatanisho wa sarufi, matumizi yasiyofaa ya vivumishi, na matumizi ya Sheng'. Hali hii iliathiri mawasiliano na kushusha hadhi ya lugha rasmi jambo linalofaa kurekebishwa. Utafiti huu ulitoa mapendekezo mbalimbali mathalan: Pana haja ya kutambua na kulinda mchango wa kikatiba kuhusu Kiswahili na vyombo vya habari. Pana umuhimu pia wa kuhakikisha kuwa lugha sanifu ya Kiswahili inazingatiwa katika mchakato huu wa utekelezaji wa katiba mpya. Aidha kuna umuhimu wa kuibua mbinu mwafaka za kuhifadhi hadhi ya Kiswahili hasa katika vyombo vya habari na nyanja zingine za kimawasiliano nchini Kenya. Sera maalum zinahitaji kubuniwa kuhakikisha kuwa mawasiliano kwa umma kupitia lugha ya Kiswahili ni sanifu na sahihi. Matumizi ya lugha hii katika vikao rasmi yanafaa kupanuliwa. Vyombo vya kukuza na kupanua msamiati wa Kiswahili vinafaa kubuniwa bila kuchukua muda mrefu. Imedhihirika kuwa vyombo vya habari vinaweza kuwa na mchango muhimu katika kutekeleza maazimio haya kwa sababu vinawafikia watu wengi.

**Utangulizi**

Vyombo vya habari vinatekeleza majukumu mengi katika jamii. Hata hivyo jukumu la kimsingi ni kupasha habari kwa hadhira pana inayosikiliza. Kufanikisha jukumu hili kwa umma ni muhimu kuzingatia lugha sanifu na sahihi (Walibora, 2001; Makoti, 2007). Sababu ya kutumia lugha sanifu ni kufanikisha upashaji wa habari kwa watu wote. Kutokana na hali hiyo, vyombo vya habari vina jukumu la kimsingi la kutumia lugha sanifu katika utoaji wake wa habari. Aidha, kutokana na upana wake wa hadhira vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja (Mohochi, 2006). Wataalamu wengi wa lugha vilevile wanaviamini kuwa kama nyenzo ya kukuza lugha (Chimerah, 2000; Kihore, 2001; Mulokozi, 2003).

Siku za hivi karibuni kumekuwa na vyombo vingi vya habari. Hali hii imechangiwa na uhuru wa wanahabari uliotolewa na serikali kuanzia mwaka wa 2002. Serikali ya rais Mwai Kibaki iliyochukua hatamu wakati huo iliahidi kupanua nafasi ya kidemokrasia, uhuru wa mtu binafsi, na haki za kimsingi za binadamu. Hali hii ilipelekea kuongezeka kwa vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha mbalimbali kama vile lugha za Kienyeji, Kiswahili na Kiingereza. Umiliki wa vyombo hivi pia uliweza kuwa wa watu binafsi kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Kasi na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano yaani teknohama katika karne ya 21 pia vilichangia mabadiliko katika asasi za kijamii ikiwepo lugha ya Kiswahili. Teknolojia hii mpya ya habari na mawasiliano, ilirahisisha mawasiliano kiasi kwamba dunia imekuwa kama kijiji kidogo. Habari na mawasiliano katika enzi zetu, ndizo dhana zinazowashughulisha walimwengu kuliko wakati mwingine wowote wa kihistoria. Maendeleo haya ni muhimu na yanafaa kuwawezesha wanadamu kutengamano na kupata maarifa mapya yanayoibuka ulimwenguni. Umuhimu wake hata hivyo hauwezi kuafikiwa kwa kikamilifu ikiwa sera na sheria za kitaifa hazitatoa uhuru wa uwasilishaji na upataji wa habari. Mataifa mengi yamekuwa na sheria finyu ambapo vyombo vya habari na habari zenyewe zinadhibitiwa na utawala jambo linalokandamiza maendeleo. Nchini Kenya, uzinduzi wa katiba mpya katika mwaka wa 2010, ulizua mwamko mpya kwa kupanua uhuru wa wananchi wote kupitia marekebisho yaliyotambua haki za mtu binafsi na maongozi kwa jumla. Vyombo vya habari vilipata msukumo mpya kutokana na vifungu kadha vya kikatiba. Lugha ya Kiswahili haikubakia nyuma katika mchakato huu wa kikatiba. Kiswahili kilitambuliwa kimbele kama lugha rasmi nchini Kenya na vilevile kutambuliwa kama lugha ya taifa. Wataalamu na wapenzi wa lugha ya Kiswahili wanaendelea kuhoji kuhusu mafanikio ya Kiswahili miaka minne baada ya uzinduzi wa katiba mpya na kuchunguza iwapo kuna hatua muhimu inayopigwa na vyombo vya habari katika matumizi sahihi ya Kiswahili

**Suala la Utafiti**

Uzinduzi wa katiba mpya nchini Kenya mnamo mwezi wa Agosti, mwaka wa 2010 ulikuwa hatua muhimu katika kubadilisha mfumo wa uongozi, jamii na hata siasa. Wananchi wa Kenya kupitia kura ya maamuzi walipitisha katiba mpya kuambatana na maono yao kama wananchi wa taifa huru. Mengi yaliweza kubadilika serikalini kutokana na azimio hili kama vile ugatuzi wa serikali, asasi ya mahakama, uwakilishi wa ubunge na utawala. Lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi mpya kupitia katiba hii mpya ambapo sasa ni mojawapo wa lugha rasmi. Awali Kiswahili kilikuwa lugha taifa pekee. Kuteuliwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi kuna maana kuwa matumizi yake inafaa kuwa sahihi na sanifu. Kutokana na matumizi mapana ya Kiswahili hasa katika vyombo vya habari, palikuwa na haja ya kuchunguza iwapo matumizi sahihi na sanifu yanazingatiwa kuambatana na vipengele vya katiba mpya la sivyo kujua makosa yanayotokea na namna ya kuyarekebisha, suala lililopelekea uchunguzi huu.

**Malengo ya Utafiti**

1. Kuchunguza athari za katiba mpya kwa lugha ya Kiswahili
2. Kuchanganua makosa ya Kiswahili yanayofanywa katika vyombo vya habari
3. Kupendekeza namna ya kurekebisha makosa hasa katika vyombo vya habari.

**Maswali ya Utafiti**

1. Katiba mpya ya Kenya imeathiri vipi matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari?
2. Kuna aina gani ya makosa inayofanywa katika vyombo vya habari?
3. Je, pana njia zozote mwafaka za kurekebisha makosa katika vyombo vya habari?

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia uchanganuzi wa kithamano kwa mujibu wa Kasomo (2007). Utafiti wa kithamano hufafanua hali halisi ya masuala yanayotafitiwa, maelezo yaliyopo kuhusiana na dhana, uchanganuzi, uainishaji, pamoja na ukadiriaji wa data. Robson (1993) anasema kuwa uchanganuzi wa kithamano hutoa mwongozo rahisi na sahili katika utafiti wa dhana, mielekeo na imani. Pia mpango wa aina hii wa utafiti huweza kutumiwa kuchunguza data inayoweza kuwakilisha idadi kuu ya watafitiwa. Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza makosa yaliyokuwa tayari yametokea kwenye vyombo vya habari zinazosomwa kwenye redio na athari zake kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Idhaa za *redio citizen* na idhaa ya taifa (KBC) ziliteuliwa kwa vile zote hutumia Kiswahili kwa saa 24 na kwamba hupokelewa kote nchini. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi makosa kwa mujibu wa Corder (1967) ambayo inaainisha makosa, kuyaweka kwenye makundi na kutambua vyanzo vyake. Mambo haya yalihitaji kuchunguzwa jinsi yalivyo huku athari zake zikifafanuliwa na kuchanganuliwa ili kueleweka bayana. Vifaa vilivyotumika kuafikia azimio hili ni pamoja na jedwali la tathmini na hojaji.

**Jedwali la Tathmini**

Uchanganuzi wa makosa kwenye taarifa za habari ulifanywa kwa kutumia jedwali la tathmini, ili kuhakikisha kwamba makosa yote katika nakala za taarifa za habari yalinukuliwa. Mtafiti alinasa taarifa za habari zilizolengwa kwa muda wa miezi mitatu za saa saba mchana na saa moja jioni kwenye kanda huku akitumia kinasa sauti. Kisha alitumia kalamu na daftari ili kunukuu taarifa za habari na baadaye kuzipiga chapa kwenye taraklishi na kutoa nakala. Mtafiti alipitia kila nakala ya taarifa na kutambulisha makosa yaliyokuwepo, kuyaainisha na kuyachanganua. Kifaa hiki ni muhimu katika shughuli hii ili kuhakikisha kuwa majopo yote ya makosa yalishughulikiwa ipasavyo. Makosa haya yaliwekwa kwenye majopo maalum kama vile kuchanganya ndimi, kutumia sheng' na kutumia upatanisho usiofaa wa kisarufi. Uchunguzi huu ulisaidia kuainisha makosa mbalimbali na kuyaweka kwenye sehemu zilizofaa. Kathuri na Pals (1993) wanasema kuwa jedwali la tathmini huwa na dhana ambazo watafitiwa huelewa kwa haraka na kutoa maoni yao kwa wepesi kuliko hojaji wazi.

**Hojaji**

Hojaji maalum iliyowalenga watangazaji wa habari kwenye mashirika mawili ya habari yaani; Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) na Idhaa ya *Redio Citizen* ilitumiwa. Hojaji hii iliongozwa na malengo ya utafiti na ilikuwa na sehemu tatu maalum. Sehemu ya kwanza ilikuwa na maswali ya jumla kuhusu mtafitiwa, sehemu ya pili ilijumuisha maswali ya kuainisha makosa kwenye taarifa za habari na sehemu ya tatu ilihusu makosa yanayoweza kuathiri mawasiliano. Hojaji hii ilikuwa na umuhimu wa kuchunguza chanzo za makosa kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makosa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Athari ya Katiba Mpya kwa Lugha ya Kiswahili**

Katiba mpya ya Kenya ilizinduliwa katika mwezi wa Agosti, mwaka wa 2010 baada ya kura ya maamuzi iliyofanyika nchini. Umuhimu wa katiba hii hauwezi kutiliwa shaka. Sababu ni kuwa katiba hii imesababisha mabadiliko makubwa katika uongozi na nyanja zote za maisha. Sura ya pili ya katiba ya Kenya, ibara ya 7 (1) inataja kuwa lugha ya taifa ya Kenya itakuwa Kiswahili. Ibara ya 7 (2) inataja kuwa kutakuwa na lugha rasmi ambazo ni Kiswahili na Kiingereza. Ibara ya 7(3) nayo inataja kuwa taifa litakuza na kulinda lugha za kienyeji nchini pamoja na kukuza na kueneza matumizi yake kwa lengo la kimawasiliano. Vifungu hivi vimeweka hadhi mpya kwa lugha ya Kiswahili na kukipatia nafasi ya kipekee katika taifa. Kiswahili kimepewa kipaumbele kwa kutajwa kimbele kama lugha rasmi. Aidha Kiswahili sasa kina majukumu mawili muhimu mathalan: lugha taifa na lugha rasmi. Yafaa ikumbukwe kuwa lugha taifa huwaunganisha wananchi wa taifa husika. Inakuwa kama kitambulisho au bendera ya taifa. Inaleta uzalendo na kufanikisha mawasiliano baina ya wananchi wote wa nchi husika. Lugha rasmi kwa upande wake hutumiwa katika vikao vyote vya kiafisi ikiwemo uandishi wa barua rasmi,

bunge, mahakama, afisi za serikali na mikutano rasmi ya kitaifa na kimataifa. Majukumu yote mawili ya lugha taifa na lugha rasmi yanafaa kutekelezwa na lugha ya Kiswahili kikatiba licha ya kuwa lugha ya Kiingereza imetajwa katika nafasi ya pili kama lugha rasmi. Jambo hili lina maana kwamba kwa sasa nchi ya Kenya ina lugha mbili rasmi. Aidha sera ya lugha nchini Kenya wakati wa uhuru, ilitawaliwa na kamati mbalimbali za elimu kama vile ripoti ya Ominde ya 1964 ambayo ilipendekeza matumizi ya Kingereza kama lugha ya kufundishia shuleni huku Kiswahili kikiwa somo katika shule za msingi, suala lililoendeleza udhalilishaji wa lugha ya Kiswahili.

Ripoti zingine kama vile ile ya Gachathi (1976), Kamunge (1988) hazikuleta mabadiliko yoyote ya kutajika kuhusu sera ya lugha nchini. Ripoti ya Mackay ya 1981 hata hivyo, ilileta mageuzi makubwa katika elimu kuhusu sera ya lugha ambapo lugha ya Kiswahili ilifanywa somo la lazima kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne katika shule za msingi na upili mtawalia. Somo hili pia liliweza kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne na darasa la nane. Jambo hili lilichangia kuimarisha hadhi ya lugha hii na kubadilisha mielekeo hasi iliyokuwepo hapo awali. Kamati ya Koech ya 1999 ilitambua lugha ya Kiswahili kama mojawapo wa masomo ya lazima katika shule za humu nchini, yaani shule za msingi, upili na vyuo vya walimu wa shule za msingi. Hili lilimaanisha kuwa wanafunzi katika shule za humu nchini walitakiwa kufuzu vizuri katika mitihani ya Kiswahili. Jambo hili kwa upande mwingine lilikuza ujuzi wa Kiswahili miongoni mwa wakenya wengi na kubadilisha mitazamo hasi waliokuwa nayo. Vitabu vingi vya Kiswahili vilizidi kuchapishwa na mashirika mbalimbali ya uchapishaji ili kutosheleza mahitaji. Vyombo vya habari navyo vikaendeleza matumizi ya Kiswahili kwa sababu vilipata wataalamu wengi waliobobea somo hili.

Uzinduzi wa katiba mpya katika mazingira haya ulichangia kuimarisha lugha ya Kiswahili na utendakazi wake. Kiswahili kilitarajiwa kutumika kwenye mawasiliano rasmi kama vile bungeni, mahakamani na pia kwenye baraza la mawaziri kama lugha ya mawasiliano. Ilitarajiwa pia kwamba stakabadhi muhimu zingeandikwa kwa lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza jambo ambalo halijafanyika. Licha ya hatua hizi muhimu ni kinaya kwamba miaka minne tangu kuzinduliwa kwa katiba mpya mengi hayajafanywa kufanikisha azimio hili. Mifano inayodhibitisha hoja hii ni mingi. Katika sherehe za kitaifa kwa mfano hotuba za rais husomwa kwa Kiingereza. Rais hutoa hotuba yake kwa Kiingereza kwa muda mrefu kisha baadaye anagusia mambo machache kwa Kiswahili jinsi ilivyokuwa awali hata kabla ya katiba mpya. Hali hii inakanganya kwa sababu lugha ya Kiswahili inaonekana kushikilia nafasi duni kiutekelezi. Ishitoshe viongozi wengine wa kiserikali hupuuza kabisa matumizi ya Kiswahili katika mawasilisho yao. Mfano mzuri ni majaji, wakurugenzi wa makampuni, maseneta na mawaziri wa serikali. Aidha mambo haya hufanyika maksudi au kwa kukosa umilisi wa lugha hii. Isitoshe, wanaojaribu kutumia Kiswahili hukiuka karibu sheria zote za mawasiliano na kuwaacha wasikilizaji na kero mioyoni. Gazeti la Kiswahili nchini bado ni moja yaani *Taifa Leo*. Jambo hili ni tofauti na hali ilivyo Tanzania ambapo kuna magazeti mengi ya Kiswahili. Aidha hakuna halmashauri yoyote iliyozinduliwa ya kukuza lugha ya Kiswahili au msamiati wake kama ilivyo katika taifa la Tanzania. Mambo haya yanadhihirisha utepetevu uliopo katika kuhakikisha utekelezaji kamili wa Kiswahili. Inaonekana kwamba, wataalamu wa Kiswahili na wapenzi wake hawana budi ila kuendelea kutetea nafasi ya Kiswahili hadi utekelezaji kamili wa kikatiba uafikiwe.

**Lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari**

Lugha ya Kiswahili imenufaika kutokana na matumizi yake katika vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni nyenzo zinazotumiwa kupeleka habari kwa watu wengi. Kuna aina tatu ya vyombo vya habari. Kuna machapisho kama vile magazeti na majarida. Kuna vyombo vya utangazaji kama redio na runinga na kuna vyombo vya mtandao vikiwemo taraklishi simu ya rununu na mitandao ya jamii. Jukumu la vyombo vya habari ni kukuza, kuendeleza na kusambaza lugha ikiwemo lugha ya Kiswahili kama anavyosema Mohochi (2006). Lugha ya Kiswahili imekuwa ikikua na kusambaa kwa kasi kupitia vyombo hivi vya habari. Aidha vyombo vya habari huhifadhi utamaduni, huendeleza mienendo mipya, mavasi na mielekeo mbalimbali katika jamii. Lugha huwa nyenzo muhimu katika utekelezaji wa masuala haya. Jambo hili limechangiwa na mambo kadha yakiwemo maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mabadiliko haya yamezua haja ya ukuaji wa lugha ili kuiwezesha kuwasilisha dhana mpya katika maisha ya kila siku kama anavyosema King'ei (2000).

**Athari ya Katiba Mpya kwa Vyombo vya Habari na Jinsi Itakavyoathiri Kiswahili.**

Uzinduzi wa katiba mpya umeleta mabadiliko mengi katika vyombo vya habari kama ulivyoathiri asasi zingine za kijamii. Sura ya nne ya katiba mpya inatoa haki za kimsingi za binadamu ambazo zinapaswa kutolewa kwa kila mwananchi bila masharti yoyote. Ibara ya 19:3 inasema hivi: "haki na uhuru wa kimsingi wa binadamu katika sehemu hii hazitolewi na serikali bali humilikiwa na kila mtu na kwamba haziwezi kupokonywa mwananchi yeyote wala kukiukwa." Sura hii ndiyo imetoa uhuru mwingi kwa wana habari kama inavyodhihirika katika ibara ya 34: 1,

2, 3, 4, na 5. Sehemu hii inatoa uhuru wa vyombo vya kielektroniki, uchapishaji na utangazaji kwa jumla wa kutangaza na kutafuta habari kwa umma bora tu wawajibikie ibara ya 33 (2) ambapo haki zao za kikatiba hazifai kukiuka haki za wananchi wengine kwa kuripoti habari zisizo sahihi au kuwaharibia sifa. Ibara ya 34 (3) imetoa uhuru wa kuanzisha na kumiliki vyombo vya utangazaji kwa watu binafsi ambazo hazifai kuingiliwa na serikali bora tu zipewe leseni. Vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali pia vimepewa uhuru wa kuhariri, na kukusanya habari zake bila kuingiliwa na zinaruhusiwa kutangaza kwa usawa kuhusu masuala yote yanayoathiri jamii. Vipengele vya 1, 2, na 3 katika ibara ya 35, vimetoa haki ya kupata habari inayohifadhiwa na serikali au mtu binafsi. Mtu yeyote pia ana uhuru wa kukosoa ujumbe wowote wa uwongo uliotolewa kumkashifu.

Sehemu hii ya katiba ina umuhimu mkubwa kwa vyombo vya habari na jinsi vinavyoendeleza taaluma yao. Hapo awali hali ilikuwa tofauti ambapo serikali ilikuwa na udhibiti mkubwa kuhusu yale ambayo yangeandikwa au kuwasilishwa. Leseni kwa vyombo vya habari zilikuwa adimu. Mabadiliko haya ya uanahabari katika katiba ya Kenya yameathiri pakubwa maendeleo yake pamoja na matumizi ya lugha. Tayari zaidi ya leseni 38 za redio zimetolewa humu nchini na bado zinaendelea kutolewa. Vituo vya runinga pia vinazidi kupanuka. Tayari kuna zaidi ya vituo kumi na vitano vilivyopewa leseni vikiwemo *Kenya Broadcasting Corporation (KBC), Nation Television (NTV), Kenya Television Network (KTN), Citizen TV, Kass TV, QTV, Sayare TV* miongoni mwa vingine. Redio kwa upande wake haijabaki nyuma huku zaidi ya leseni 38 zikiwa tayari zimetolewa humu nchini kama ilivyotajwa. Baadhi ya vituo vya redio vinatangaza kwa Kiswahili kwa saa 24 kama vile *Redio citizen, KBC Redio Taifa, Redio Jambo, Milele fm, Redio Umoja, Baraka fm, na Pwani fm*. Yafaa ifahamike kwamba hata zile stesheni za radio ambazo hazitumii Kiswahili pekee bado hutoa baadhi ya matangazo kwa lugha hiyo. Kutokana na mabadiliko haya basi, lugha ya Kiswahili ina nafasi nzuri na muhimu ya kuendelea na kukua kuliko wakati mwingine wowote ule. Tayari Kiswahili ndiyo lugha ya matumizi ya muungano wa Afrika Mashariki na kigezo kimoja cha mataifa wanachama ni kukuza na kutumia lugha ya Kiswahili.

Changamoto kubwa katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili pamoja na kuieneza kwa kasi inayokwenda ni uzingatifu wa lugha fasaha na sanifu. Yafaa ifahamike kwamba lugha rasmi yafaa iwe sanifu. Tayari kuna ushahidi mwingi unaodhihirisha kuwa viwango vya Kiswahili sanifu vinazidi kushuka hasa katika vyombo vya habari. Makosa mengi ambayo hayafai kufanywa yanatokea kwenye vyombo vya habari hasa kwenye redio na runinga za humu nchini na kuzua wasiwasi mwingi miongoni mwa wataalamu. Mashirika mengi ya habari yaliyopewa leseni yanaweza kuwa hayazingatii viwango bora vya lugha kwa sababu mbalimbali. Yanaweza kuwa yanawaajiri wanagenzi ambao hawana umilisi wa lugha kwa vile wataridhika na mshahara mdogo tofauti na wenzao walio na tajriba ya juu. Vilevile kuna wengine wanaoweza kuwa wanavutiwa na faida bila kujali masrahi mengine kama matumizi ya lugha sanifu au fasaha katika utangazaji. Hali hii ni tisho na inafaa kudhibitiwa. Sehemu ifuatayo inatoa mifano ya makosa katika vyombo vya habari kushadidia kauli hii.

**Makosa ya Lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari**

Makosa kadhaa yalidhihirika ambayo hayafai kutokea ikiwa mawasiliano kamili yataafikiwa kupitia vyombo vya habari. Baadhi ya makosa yaliyotolewa hapa yalipatikana katika idhaa za *Redio Citizen* na *Idhaa ya Taifa* kwenye taarifa za habari.

**A. Makosa ya Kuchanganya Ndimi**

Uchanganyaji ndimi ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika wakati mmoja aidha kwa kukosa msamiati mwafaka au maksudi ili kuafikia lengo la kimawasiliano. Aidha kutokana na utamaduni, msemaji anaweza anaweza kushindwa kutaja baadhi ya dhana kwa Kiswahili kwa sababu ni mwiko kuzitaja hadharani. Mbaabu (1995) anasema kuwa uchanganyaji ndimi pia hutumiwa wakati wa kuzungumzia mambo ya siri ambapo wahusika hawataki wengine washiriki. Licha ya maoni haya tofauti ya wataalamu, uchanganyaji wa ndimi haukubaliki katika matumizi sanifu ya lugha na unapotokea katika muktadha rasmi unakuwa ni makosa. Makosa ya aina hii yalidhihirika katika baadhi ya taarifa za habari zilizotafitiwa kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

1a…gari hilo aina ya **pick up…** redio citizen 3/4/14
2a…ikifuatiwa na **rift valley…** redio citizen 3/4/14
3a…watu wanne walithibitishwa kufa miongoni mwao **turnboy** wa trela… redio citizen 14/12/14
4a…jaji mkuu **dr.** Willy Mutunga… redio citizen 12/12/13
5a…wafanyikazi wa maduka ya **supermarket** ya Tuskys…20/12/13

**Sentensi sahihi**

1b…gari hilo la **kubebea mizigo**

2b…ikifuatiwa na eneo la bonde **la ufa**
3b…watu wanne walithibitishwa kufa miongoni mwao **utingo** wa trela
4b…Jaji mkuu **dkt**. Willy Mutunga
5b…wafanyikazi wa **maduka ya jumla** ya Tuskys

B. **Matumizi Yasiyofaa ya Akronimu za Kiingereza**

Akronimu ni vivupisho vya maneno yanayotumiwa kuwakilisha neno kamili. Huwa mbinu maalum katika uundaji wa istilahi katika lugha. Kila lugha huwa na akronimu zake. Hata hivyo, wakati akronimu za Kiingereza zinapotumika katika muktadha wa mawasiliano ya Kiswahili yanakuwa makosa kwa vile wasomaji wanaweza kupata tafsiri isiyofaa. Baadhi ya makosa ya aina hii ni kama yafuatavyo**:**

6a…**OCPD** wa Embu… redio citizen 28/12/13
7a…shirika la **IGAD** lachukua msimamo mkali dhidi ya Sudan … redio taifa 27/12/13
8a…amekiri kwamba wanajeshi wa **KDF** hawataondoka nchini Somalia… redio citizen 4/4/14
9a…idara ya **CID**… redio citizen 27/11/13
10a…majaji wa **ICC** wameipa serikali ya Kenya muda… redio citizen 10/12/13
11a…tume ya **IEBC**…redio taifa 19/12/13
12a… halmashauri ya **NACADA**…redio taifa 28/12/13

**Makosa haya yangekosolewa kama ifuatavyo:**

6b mkuu wa polisi katika eneo la Embu
7b…shirika la kiserikali la maendeleo katika eneo hili (**IGAD**) lachukua msimamo mkali kuhusu Sudan
8b…amekiri kwamba wanajeshi wa ulinzi wa Kenya (**KDF**) hawataondoka nchini Somalia
9b…idara ya polisi inayopeleleza vitendo vya jinai (**CID**)
10b…majaji wa mahakama ya kimataifa kuhusu uhalifu na vitendo vya jinai (**ICC**)
11b…tume huru ya uratibu wa mipaka na uchaguzi (**IEBC**)
12b…halmashauri ya kitaifa inayopambana na pombe na dawa za kulevya (**NACADA)**

**C. Matumizi Yasiyofaa ya Vivumishi vya Pekee**

Vivumishi vya pekee hutumiwa kuelezea sifa zaidi za nomino kwa njia mbalimbali. Kuna aina tano ya vivumishi vya pekee mathalan: **enye**, **enyewe**, **ote o-ote**, na **ingine**. Vivumishi hivi huwa na dhima tofauti kulingana na matumizi yake. **Enye** huonyesha umiliki. **Enyewe** husisitiza, kuhusu jina au kitu kinachorejelewa, **ote** huonyesha ujumla wa vitu huku **o-ote** ikileta maana ya kutobagua na **ingine** ikionyesha dhana ya zaidi ya. Ikiwa kivumishi kimoja kitachukua nafasi ya kingine katika muktadha usiofaa basi maana itabadilika na kosa la kisarufi litakuwa limefanyika. Mifano ifuatayo ilidhihirisha makosa ya matumizi yasiyofaa ya vivumishi vya pekee:

13a…huku Omar akijifunga **mwenyewe**…redio taifa 5/4/14
14a…mtu **mwenye** ameaga dunia usiku wa kuamkia leo… redio citizen4/4/14
15a…serikali yasambaza mbolea **kwenye** vituo vyote **ya** halmashauri…redio taifa 21/12/13
16a…washambuliaji hao walisemekana kuifyatua risasi kadhaa ^ nyumba ya waathiriwa redio taifa.11/12/13

Sentensi hizi zingesahihishwa kwa njia ifuatayo:
13b…huku Omar **mwenyewe** akifunga bao kwenye lango lao
14b…mtu ali**yea**ga dunia usiku wa kuamkia leo
15b…serikali yasambaza mbolea kwenye vituo vyote **vya** halmashauri
16b…washambuliaji hao walisemekana kufyatua risasi kadhaa **kwenye** nyumba ya waathiriwa.

**D. Ukosefu wa Upatanisho wa Kisarufi**

Upatanisho wa sarufi huleta uwiano kati ya nomino na maneno mengine hasa vitenzi na vivumishi. Upatanisho huu hulingana na ngeli ya nomino pamoja na kivumishi au kitenzi. Mbaabu (1995) anasema kuwa ngeli ndio uti wa mgongo wa sarufi ya Kiswahili na makosa hutokea mara tu viambishi visivyofaa vinapotumika katika sentensi. Aidha Ontieri (2010) anaunga mkono kauli hii kwa kusema kuwa kukiukwa kwa upatanishi wa kisarufi huleta mgongano kati ya nomino na vitenzi au kati ya nomino na vivumishi. Vivumishi hutoa habari zaidi kuhusu nomino katika sentensi. Mifano ifuatayo ilidhihirisha makosa katika matumizi ya vivumishi:

17a….huku ikisema matakwa ya wahudumu **za** sekta ….redio taifa 18/12/13
18a…..Bomu la kutegwa kwenye gari karibu na mkahawa mmoja katikati mwa Iraq **umewaua** takriban watu wanne…redio taifa 9/12/13

19a….baada ya kuishinda Nairobi City Stars **mbao mawili** kwa bila…..26/12/13
20a….kocha wa kilabu **hiyo**…..redio taifa 4/1/14
21a….bandari kuu **wa** Mombasa…2/1/14
22a maafisa **ya** utawala….redio citizen 23/11/13
23a….waya **wa** stima….. redio citizen 26/11/13

Mifano iliyotajwa inafaa kusahihishwa kama ifuatavyo:
18b huku ikisema wahudumu **wa** sekta….
19b….bomu la kutegwa kwenye gari karibu na mkahawa mmoja katikati mwa Iraq **limewaua** watu wanne
20b….Baada ya kuishinda Nairobi City Stars **mabao mawili** kwa bila…..
21b….kocha wa klabu **hicho**…..
22b…..bandari kuu **ya** Mombasa
23b….maafisa **wa** utawala
24b…waya **ya** stima….

E. **Matumizi ya Sheng'**
Sheng' ni kilugha cha vijana kinachotumiwa kwa mawasiliano baina yao. Mbaabu (1996) anasema kuwa Sheng' hutumia sintaksia ya Kiswahili na kukopa msamiati wake kutoka lugha mbalimbali kama vile Kiingereza na lugha za kienyeji za humu nchini. Sheng' imekuwepo tangu miaka ya themanini ilipoanza katika mitaa ya Eastlands. Athari zake kwa lugha rasmi ni wazi na baadhi ya vyombo vya habari huitumia maksudi ili kuvutia hadhira hasa ya vijana. Matumizi yake hupatikana zaidi katika matangazo ya kibiashara ambapo tunapata mifano ya kauli zifuatazo:

25a…**Lipua** mamilioni
26a…**Kwachua** mamilioni
27a…**Bambika** na tusker
28a…Pesa **pap**
29a…**Blue band** ya kadogo

Kauli hizi iwapo zingeandikwa kwa lugha sanifu zingefaa kuandikwa kama ifuatavyo:
25b…**jishindie** mamilioni ya pesa
26b…**pata** mamilioni
27a…**burudika** na pombe ya tusker
28a…pata pesa **mara moja**
29a.. **siagi** ile ndogo

**Mahitimisho**
Makala hii imechunguza mchango wa katiba mpya katika kukuza na kuimarisha lugha ya Kiswahili hasa katika vyombo vya habari. Imebainika kwamba katiba ya Kenya ya 2010 imekipatia Kiswahili majukumu mawili ya kuwa lugha taifa na lugha rasmi. Majukumu haya yanakipatia Kiswahili nafasi ya pekee miongoni mwa lugha za Kenya.
Aidha asilimia 70 ya wakenya hutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano kwa mujibu wa Sande (2010). Kiswahili sasa kina nafasi ya kipekee ya kupanuka, kuenea na kukua kwa mwendo wa kasi kote nchini Kenya, na ulimwengu mzima kwa jumla. Vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuafikia azimio hili kwa sababu vinawafikia watu wengu kwa wakati mmoja. Aidha vimepewa mamlaka ya kikatiba ya kupata habari na kuzieneza bila vikwazo tofauti na ilivyokuwa awali. Kutokana na uwezo huu wa kikatiba, vyombo vya habari vimepewa leseni ya utangazaji humu nchini. Mchango wao katika kukuza, kueneza na kuimarisha lugha ya Kiswahili ni muhimu na unafaa kuungwa mkono. Makala hii hata hivyo imetoa tahadhali kwamba makosa mengi yanatokea katika vyombo vya habari na yanafaa kurekebishwa. Baadhi ya makosa yaliyotajwa ni kama kuchanganya ndimi, kutumia Sheng', matumizi yasiyofaa ya vivumishi na kukosa upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Matumizi ya lugha sanifu yatahifadhi hadhi yake na kufanikisha mawasiliano huku wanafunzi na wasomi wa Kiswahili wakifaidika kwa kujifunza hasa kupitia vyombo vya habari.

**Mapendekezo**
Kufanikisha hadhi mpya ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya kunahitaji juhudi za maksudi kwa wadau wote wanaohusika mathalan: serikali, vyombo vya habari, wataalamu, wakuza mitalaa na hata wananchi kwa jumla. Sera mpya ya lugha inafaa kubuniwa na kuanza kutekelezwa ikiongozwa na mabadiliko ya kikatiba. Nyaraka muhimu za serikali zinafaa kutafsiriwa kwa Kiswahili. Maafisa wakuu wa serikali wanafaa kushinikizwa kutumia

lugha zote mbili katika hotuba zao kwa kukipa kipaumbele Kiswahili kutokana na majukumu yake mawili. Hali hii inafaa kuimarishwa kwa sababu viongozi ni vielelezo kwa wengine. Aidha halmashauri ya kuhakikisha matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili imezingatiwa katika vyombo vya habari, bunge na hata kwenye machapisho mbalimbali inafaa kubuniwa. Inafaa kuwa na mkurugenzi wa kukuza na kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini kwa kuhamasisha wafanyikazi na wananchi kwa jumla. Utafiti zaidi unafaa kufanywa kuhusu mielekeo ya wakenya kuhusu lugha ya Kiswahili hasa baada ya uzinduzi wa katiba mpya. Uchunguzi pia unahitaji kufanywa kuhusu sera za lugha zinazotawala vyombo chipukizi vya utangazaji ili kupata taswira halisi ya mambo kwa lengo la kuimarisha matumizi sahihi ya Kiswahili nchini.

**MAREJELEO**


Chimerah, R. 2000. Kiswahili: Past, Present and Future. Nairobi: Nairobi University Press.

Corder, S.P. 1967. The Significance of Learners Errors. London: Oxford University Press.

Kasomo, D. 2007. Research Methods in Humanities and Education. Eldoret: Zapt Chancery.

Kathuri, N.J. na Pals, D.A. 1993. Introduction to Education Research. Egerton: Education Media Center.

Kenya Law Report 2010 Laws of Kenya: The Constitution of Kenya. Nairobi: National Council for Law Reporting.

Kihore, Yared, M. David, P.B. Massamba na Yohana P. Msanjila. 2001. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu SAMAKISA. Dar es Salaam: TUKI

King,ei, K. 2000. Matatizo ya Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya katika Swahili Forum, AAP 64:45-56

Makoti, V.S. 2007. Matumizi ya Kiswahili Nchini Kenya katika Redio na Runinga. Katika Njogu, K. Mh Kiswahili na Elimu Nchini Kenya. Nairobi: Twaweza communications.

Mbaabu, I. 1995. Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili. Nairobi: Longhorn.

Mbaabu, I. 1996. Language Policy in E. Africa. Nairobi: ERAP.

Mohochi, E.S. 2006. Kiswahili na Vyombo vya Habari Nchini Kenya: Matumizi na Makosa katika Matumizi ya Lugha: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 69:52-61.

Mulokozi, M. 2003. Kiswahili as a national and International Language. Dar es Salaam: TUKI.

Ontieri, J.O. 2010. Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuuu cha Egerton.

Robson, C. 1993. Real World Research; a Resource for Social Scientists and Practioner-Researchers. Oxford: Blackwell Publishing Company.

Sande, S. 2010. Kenya: New Constitution Provides for Kiswahili as the Second Official Language after English. In: www.newsfromafrica.org/articles/art.com. tarehe ya upakuzi 20/10/14.

Walibora, K.W. 2001. Matatizo Ya Tafsiri katika Vyombo vya Habari katika Kihore, Y.M. Mh Kiswahili 64 Dar es Salaam: TUKI. uk. 23.